

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**

Simu: +255-26-2323189

Barua pepe: [ps@moha.go.tz](mailto:ps@moha.go.tz)

Tovuti: [www.moha.go.tz](http://www.moha.go.tz)



Mji wa Serikali - Mtumba,

Mtaa wa Habari/Afya

S. L. P. 2916,

40483 DODOMA.

13 Julai, 2023.

**TAARIFA KWA UMMA**

**UTEUZI WA WAJUMBE WA BODI YA PAROLE**

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mhandisi Hamad M. Y Masauni (Mb), kwa Mamlaka aliyonayo chini ya Kifungu cha 3(2)(f) cha Sheria ya Bodi za Parole, Sura 400 Rejeo la 2002 amewateua **Jaji Mstaafu John Samuel Mgeta** na **Kamishna Jenerali Mstaafu wa Jeshi la Magereza Dkt. Juma Ally Malewa**, kuwa Wajumbe wa Bodi ya Taifa ya Parole.

Uteuzi huu unakamilisha wajumbe wa Bodi ya Taifa ya Parole baada ya baadhi ya wajumbe wa awali kumaliza muda wao. Aidha, mwezi Aprili, 2023 Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan alimteua Balozi Khamis Sued Kagasheki kuwa Mwenyekiti mpya wa Bodi ya Taifa ya Parole na kufanya Bodi hiyo kuwa na Wajumbe Wafuatao:

1. Balozi Khamis Sued Kagasheki - Mwenyekiti
2. Mzee Ramadhan Nyamka (CGP) - Katibu
3. Camillus M. Wambura (IGP) - Mjumbe
4. Prof. Tumaini Nagu (Mganga Mkuu wa Serikali) - Mjumbe
5. Coletha N. Kiwale (Ofisi ya Rais Ikulu) - Mjumbe
6. Sylvester Mwakitalu (Mkurugenzi wa Mashtaka) - Mjumbe

Imetolewa na:-

**Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi